# Tashtiti kama Mbinu ya Uwasilishaji Maudhui katika Tamthilia Iliyotafsiriwa kwa Kiswahili: Mfano wa *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*

*Nancy K. Ayodi Mokaya*
*Chuo Kikuu cha Maasai Mara*

**Ikisiri**

**Makala haya yanadhihirisha umwafaka wa tashtiti kama mbinu ya kuweka wazi na kurekebisha uovu na ujinga katika jamii kwa ucheshi. Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Gogol, 1979) iliyotafsiriwa na Mwakasaka kutoka Kiingereza hadi Kiswahili imechanganuliwa kwa misingi ya mbinu ya tashtiti. Tashtiti haiibui tu ucheshi bali ucheshi wenye lengo la kurekebisha. Nadharia Mfumo ya Highet (1962) ndiyo msingi wa makala haya. Highet anafafanua tashtiti na vipengele vyake kumi na moja ambavyo ndivyo huunda mfumo wa tashtiti. Vipengele hivi kumi na moja; ni kinaya, kweli kinzani, mwigo wa kubeza, usemi wa kimtaa, mpomoko, pujufu, vurugu, uangavu, chuku, mada za siku na tabaini. Umuhimu wa makala haya unaonyesha namna mwandishi Gogol katika tamthilia yake *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ametumia tashtiti kufanyia mzaha mambo mazito akiwa na lengo la kufichua uovu na ujinga katika jamii. Uovu kama ukiukaji sheria, vurugu na unafiki. Inatarajiwa kwamba makala haya yatapambanua tashtiti kama mbinu ya uandishi kwa lengo kuonyesha umuhimu wa mbinu hii katika kuwasilisha maudhui mazito na nyeti kwa ucheshi.**

**Maneno Muhimu:** Tashtiti, Kinaya, Kweli Kinza, Mwigo wa Kubeza, Usemi wa Kimtaa, Mpomoko.

## Utangulizi

Tashtiti ni mbinu ambayo imetumiwa na watunzi kutaja yasiyotajika bila kuchukiza, kuchukuliwa vibaya au kumwudhi msomaji. Imetumiwa na wataalamu hodari mfano, Voltaire, Rabelais, Petronius, Swift na wanamitindo bora sana kama Pope, Horace na Aristophanes. Pia, imetumiwa kama mfano bora na watu wenye akili ya uzawa kama vile Lucretius, Goeth na Shakespeare. Hata hivyo, kinyume na futuhi na tanzia, tashtiti haijashughulikiwa kwa dhati na wahakiki. Ingawa katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na dalili za ilhamu kubwa katika maandishi ya tashtiti, mtazamo hasi wa jadi (bila sababu) dhidi ya tashtiti ungalipo. Mwanatashtiti ni mharibu; huharibu kilichopo (ambacho kwa watu wengi huonekana kuwa sawa) na hajali kujaza ombwe tupu analosababisha.

Mbatiah (2000) ameeleza tashtiti kuwa ni kunga ya utunzi inayotumiwa kuyashambulia maovu ya kijamii na dosari za kitabia kama vile uzandiki; kwa kubeza na kudhihaki. Lengo la mtunzi anayetumia *tashtiti* ni kurekebisha tabia za wanadamu. Hivyo tunaweza kuzungumzia juu ya riwaya za *kitashtiti* katika riwaya kama *Rosa Mistika* ambamo mtunzi anashambulia malezi yasiyofaa ya wasichana kwa kuwabeza wazazi waliofeli mfano Zakaria.

Lengo la wasilisho hili ni kudhihirisha namna mwandishi Nikolai Gogol katika tamthilia yake *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* alivyofanyia mzaha mambo mazito ya kuchukiza akiwa na lengo la kufichua uovu na ujinga katika jamii pamoja na kuirekebisha jamii. Mbinu ya uwasilishaji ujumbe mzito wa kuchukiza kwa kucheka ni tashtiti. Highet (1962) anafafanua tashtiti na vipengele vyake kumi na moja ambavyo ndivyo huunda mfumo wa tashtiti. Vipengele hivi kumi na moja ni: kinaya, kweli kinzani, mwigo wa kubeza, usemi wa kimtaa, mpomoko, pujufu, vurugu, uangavu, chuku, mada za siku na tabaini.

## Matumizi ya Vipengele vya Tashtiti na Maudhui Yanayowasilshwa kwavyo

Baada ya kusoma tamthilia ya Gogol *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*, vipengele vifuatavyo kumi vya tashtiti vilionekana kutumika: kinaya, kweli kinzani, mwigo wa kubeza, usemi wa kimtaa, mpomoko, pujufu, vurugu, uangavu, chuku na mada za siku. Kipengele kimoja tu cha tashtiti kati ya kumi na

moja kwa mujibu wa Highet (1962), hakijatumika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* nacho ni tabaini. Ufuatao ni ufafanuzi wa vipengele kumi vya tashtiti kwa mujibu wa Highet (keshatajwa), wataalamu, mathalani Baldick (2001) miongoni mwa wengine pamoja na kuonyesha umuhimu wa kila kipengele kama mbinu ya uwasilishaji maudhui katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali.*

**Kinaya**

Baldick (2001) anaeleza kuwa, kinaya ni hali ambapo panadhihirika futuhi tatizi kiasi kwamba kauli ambayo hujitokeza kuwa ya moja kwa moja hudhoofishwa na muktadha uliopo na hubakia kuonekana tofauti kabisa. Anaendelea kueleza kwamba, kinaya kimedhihirika katika fasihi nyingi kuanzia tanzia ya Sophocles hadi riwaya za Jane Austern na Henry James. Zaidi mno, anaendelea, Kinaya ni muhimu hasa katika tashtiti za waandishi Voltaire na Swift. Baldick(*keshatajwa*) anaendelea kueleza kuwa kinaya semwa huhusu mgongano kati ya kinachosemwa na kinachomaanishwa.

Kulingana na Longsworth (1973), kinaya ni mbinu ambayo kwayo msomaji husema jambo fulani akimaanisha lingine. Kwa mfano, msemaji kimakusudi kueleza kitendo cha kijinga kuwa ni cha busara, au kumpongeza mwoga kwa ujasiri wake au kukisifu kitu chenye sura mbaya kwa uzuri au urembo wake.

Mbatiah (2000) ameeleza kwamba kinaya pia hujulikana kama stihizai. Kuna aina kadhaa ya *kinaya*. Kimsingi kinaya hutumiwa kutilia mkazo ujumbe fulani. Pia huangaza utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya jinsi mambo yanavyoonekana na jinsi yalivyo hasa katika fasihi ya *kitashtiti*.

Murungi na wenzake (2011) wameeleza kwamba, kinaya ni kinyume cha jambo au matarajio. Ni tashtiti au stihizai.

Kutokana na maelezo haya ya kitaaluma imebainika kuwa kinaya ni hali ya kuchekesha au ya ajabu ya kitu au mahali ambayo ni tofauti sana na kile kinachotarajiwa. Kwa mfano, alipopata kazi, hatimaye aligundua kuwa hakuipenda. Maana nyingine ya kinaya ni matumizi ya maneno ambayo ni kinyume na kile hasa kinachosemwa; mara nyingi huwa kama masihara au utani. Maana hii ndiyo iliyotumika katika wasilisho langu.

Ifuatayo ni mifano ya matumizi ya kinaya katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Gogol, 1979):

1) Maswali ya Anna kumhusu Mkaguzi Mkuu wa Serikali yanachekesha; auliza “Yukoje? Ana sharafa? Ni mzuri?”. Hiki ni kinaya mama na binti kupigania penzi la Ghlestakovu! Uzito wa vita hivi vya mama na binti katika suala nyeti la mapenzi unasahilishwa kwa kinaya hiki. Matokeo ni ucheshi ambao unaficha kinyaa kilichoko.
2) Ghlestakovu ala chakula kwa deni hotelini. Halipi ilhali anateta ni kwa nini yeye haongezewi kachumbari kama wateja wengine. Kinaya hiki kinachekesha kwa sababu yeye Ghlestakovu alaye kwa deni anataka vinono ambavyo watu wadogowadogo kiuchumi (awaitavyo Ghlestakovu, Mkaguzi Mkuu bandia wa Serikali) hulipia na hivyo hupewa.
3) Mkuu wa Wilaya kumrejelea Ghlestakovu kama ‘Mgeni Maarufu’ ni kinaya. Hali hii inamchekesha msomaji na mtazamaji ambao wanatambua kuwa Ghlestakovu amekosewa kuwa ndiye Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Yeye (Ghlestakovu) si mgeni maarufu. Hadhira inashuhudia kwa njia ya ucheshi upumbavu na ujinga wa Mkuu wa Wilaya na maafisa wake wote kudanganywa na Ghlestakovu.Ucheshi huu unaficha aibu iliyoko kutokana na mji wote kudanganywa na mtu mmoja ayari.
4) Mkuu wa Wilaya kujinadi kwa Ghlestakovu kuwa wao sio kama viongozi wengine wanaojali zaidi shughuli zao za binafsi bali wanajali uongozi bora na uaminifu ni kinaya. Ukweli ni kwamba, Mkuu wa Wilaya na maafisa wenzake wana ubinafsi. Kinaya hiki kinaficha hali hii.
5) Mama (Anna) anapomshtumu bintiye hivi “Tabia mbaya kama hiyo! Na wewe una watu wengi wa kuwaiga”! Ukweli ni kuwa mama hana tabia, sembuse bintiye! Mama anashindana

na bintiye kupata penzi la mgeni wao Ghlestakovu. Hali hii ya kuaibisha imeelezwa kiucheshi na kuficha fedheha anayozua mama kwa kutaka mpenzi ambaye bintiye anamtaka pia.

**Kweli Kinzani**

Baldick *(keshatajwa*) anaeleza kwamba, kweli kinzani ni kauli au matamshi ambayo kwa njia ya kushangaza mno huzua mgongano na kujikinza kiasi cha kutuchochea kuwaza juu ya muktadha mwingine ambamo hali iliyoelezwa inaweza kuwa kweli. Mfano wa kweli kinzani ni kauli 'Mtoto ndiye baba wa mwanamme'. Katika muktadha mpana, dhana kweli kinzani huweza kuelezea mtu au hali ambayo ina sifa wazi za ukinzani.

Ufafanuzi huu umeonyesha kuwa kweli kinzani ni kauli ambayo ina mawazo mawili kinzani ambayo hufanya hali kuwa isiyowezekana kamwe au isiyo ya kawaida, ingawa huenda ikawa ni kweli. Ni kweli iliyo kama uongo, neno linalooonekana kama kwamba ni la kinyume kumbe ni sahihi; fumbo la maneno. Pia mtu, kitu au hali ambayo ina sifa mbili ambazo ni kinyume na kwa hivyo kuonekana kuwa ajabu.

Kwa mfano, ni kweli inayokinza kuwa alikuwa mtu pweke aliyependa kupiga gumzo na wageni. Mfano mwingine, ni kweli kinzani kuwa baadhi ya wanafutuhi mabingwa au weledi huwa na maisha ya kibinafsi yasiyo ya furaha. Mfano wa tatu, ni kweli kinzani kuwa baadhi ya watu maskini sana huishi katika baadhi ya sehemu wanakoishi watu matajiri sana. Mfano wa mwisho, ni kweli kinzani kuwa pindi alivyojitahidi kula chakula kidogo ndivyo alivyozidi kunenepa.

Mifano ya kweli kinzani katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*:

1) Ni ukweli unaokinza Mkuu wa Wilaya kumwambia Hakimu kuwa anaweza kuisafisha mahakama yake mpaka baada ya Mkaguzi Mkuu kupita, halafu akavirudisha vitu vyote (vinavyofanya mahakama inuke) mahali pake akipenda kufanya hivyo. Kweli kinzani hii inashambulia kiucheshi hali ya kutowajibika kwa wafanyakazi ambao wanatekeleza majukumu yao kwa ajili ya kukaguliwa, baada ya kukaguliwa, wao hurejelea hali yao ya kawaida. Hali hii inawacheka wahudumu katika nyadhfa zao muhimu wasiowajibika bali huharibu na kutumia vibaya mali ya umma.
2) Ni ukweli unaokinza Bwana Posta kuambiwa na Mkuu wa Wilaya awe akisoma barua zinazopita katika Posta yake kisha kuzifunga au kuzituma hivyo zikiwa wazi. Hali hii kitashtiti inaeleza ukweli mchungu pasi kutia uchungu kwa msomaji na mtazamaji wa tamthilia. Ukweli uliopo na ambao unaelezwa kimzaha ni kuwa kuna uozo wa kupindukia katika jamii.
3) Ni ukweli unaokinza kuwa Ghlestakovu, 'Mkaguzi Mkuu wa Serikali' anaishiwa na pesa mpaka anauza nguo zake, mfano, suti yake mpya-asemavyo mtumishi wake Yosif. Hali hii inazua ucheshi mno. Ni ajabu mtu kuuza mavazi ili kujistarehesha hotelini afanyavyo Ghlestakovu. Jambo hili la fedheha limesahilishwa kwa tashtiti hii-kweli kinzani.
4) Kweli kinzani ambapo mama na binti, kila mmoja aking'ang'ana kupata penzi la Ghlestakovu ni hali ya kustaajabisha na kuudhi. Hali hii mbaya imesahilishwa kwa kweli kinzani hasa kwa usemi huu wa wahusika:

   Anna: (mamake Marya) …nilitambua kuwa alikuwa akinichungulia mara kwa mara. Marya: (bintiye Anna) Sasa mama, unajua kuwa alikuwa akiniangalia mimi. (Gogol, 1979). Hali hii ya kuchukiza na kuzua kinyaa inaelezwa kiucheshi kupitia kweli kinzani.
5) Ni ukweli unaokinza kuwa 'Mkaguzi Mkuu wa Serikali' anamuomba pesa yule anayehitajika kukaguliwa. Aibu ambayo ingemgubika mtu huyu 'maarufu' tena ombaomba inaondolewa kwa tashtiti hii. Badala yake ni ucheshi.
6) Majigambo ya Mkuu wa Wilaya kuwa bintiye ataolewa na mtu maarufu ni ukweli unaokinza. Mrejelewa si mtu maarufu na hivyo hali hii inazua kicheko. Kicheko ambacho kinacheka viongozi. Mkuu wa Wilaya anapofushwa na mnafiki Ghlestakovu, 'Mkaguzi Mkuu bandia wa Serikali'. Anapofushwa kwa kuwa na tamaa ya mali na ukuu punde bintiye atakapoolewa na mtu huyu 'mashuhuri'.

Kuwepo matumizi ya tashtiti (kweli kinzani) katika tamthilia kunaonyesha kuwa tashtiti ni mbinu mwafaka ya kuwasilisha maudhui nyeti kwa njia ya ucheshi.

**Mwigo wa Kubeza**

Baldick (*keshatajwa)* anaeleza kwamba huu ni mwigo wa kudhihaki mtindo wa kazi iliyoandikwa (zilizoandikwa) kwa kufanyia mzaha kweli, kaida za mwandishi au skuli fulani kwa njia ya bezo iliyotiwa chumvi. Mwigo wa kubeza, anaendelea, unahusiana na tashtiti inayoadhibu na pia uigaji wa mambo ya kuchekesha kwa kutumia mitindo maarufu kuelezea mada hafifu mno. Baldick(*keshatajwa*) anaendelea kwa kuandika kuwa, Aristophanes, Mgiriki mwigizaji aliiga kwa bezo mitindo ya Aeschylus na Euripides katika kazi yake *The Frogs* (405 Kabla Masiha).

Imedhihirika kuwa mwigo wa kubeza ni kifungu cha maandishi, muziki, uigizaji ambacho kimakusudi huiga mtindo wa mtu au kitu kwa ajili ya kuburudisha. Maana nyingine ya mwigo wa kubeza ni isiyoridhisha; yaani kitu ambacho ni mfano mbaya au usiofaa wa kitu kingine kiasi kuwa kitu hicho huonekana kubezwa au kudhihakiwa. Mfano ni maongezi ya kawaida kuwa polisi wanaoitisha hongo, huwa wamepandwa na 'roho mtakakitu' ni mwigo wa kubeza maandishi matakatifu 'Roho Mtakatifu' katika bibilia tukufu.

Mifano ya mwigo wa kubeza katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* :

1) Mkuu wa Wilaya anaigiza namna Mkaguzi wa Serikali atakavyouliza maswali punde atakavyoingia mfano, "Ni nani Bwana Huruma…mleteni kwangu…". Hali hii kitashtiti inaeleza ukweli pasi kutia uchungu kwa viongozi wasiowajibika. Haya maswali tarajiwa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali hayakasirishi ilhali yanarajelea wasiwasi waliyo nayo viongozi kwa kukaguliwa maana wanajua hawajatekeleza majukumu yao ipasavyo-ni kama kucheka viongozi hawa wasiowajibika.
2) Mwigo wa kubeza, "Mapenzi yako yatimie" unarejelea utundu wa mwalimu kupuuza kila anapoambiwa kuwa ufunzaji wake ni duni, daima yeye hujibu "mapenzi yako yatimie", kumaanisha atajirekebisha lakini hafanyi hivyo, hubaki vivyo hivyo. Tashtiti hii inaeleza udhaifu wa mwalimu kiucheshi, hali inayoficha ukali wa hali inayorejelewa.

Matumizi ya tashtiti hii pamoja na maudhui yaliyowasilishwa kwayo ni thibitisho kuwa kuna matumizi ya vipengele mbalimbali vya tashtiti katika tamthilia *Mkaguzi Mkuu wa Serikali.* Pili, Tashtiti imetumika kwa namna mbalimbali na mtunzi wa tamthilia kuwasilisha maudhui katika tamthilia hii. Tatu, tashtiti ina umuhimu kama mbinu mwafaka ya kuwasilisha maudhui.

**Usemi wa Kimtaa**

Baldick (keshatajwa) anaeleza kwamba usemi wa kimtaa ni matumizi ya usemi usio rasmi ambao unafaa hali ya kila siku na wala sio katika maandishi. Usemi huu ni tofauti kimatamshi, kimsamiati na kisarufi. Mfano ni usemi wa Mulili katika *Usaliti Mjini* (Imbuga, 1994:76).

Mulili: 'Wao nafikiri ni akina nani kukosa kushirikiana? Tunawalipia kwa karo yao, tunawalipia chakula yao ya raha, tunawapatianga mambo yote muhimu ...'

Usemi wa kimtaa ni neno au kifungu cha maneno ambacho hutumika katika mazungumzo lakini si katika usemi au maandishi rasmi. Ufuatao ni mfano wa usemi wa kimtaa katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*

1) Semi za kimtaa *tiptop* na *born city* zinarejelea malezi ya kudekezwa aliyopewa Ghlestakovu na wazazi wake. Malezi haya duni yanamhasiri baadaye- anafuja pesa. Hakuudhi kurejelea malezi duni kwa dhana hizi za kimtaa, *born city* na *tiptop.*

Maudhui yaliyowasilishwa kwa kipengele hiki cha tashtiti ni thibitisho kuwa usemi wa kimtaa, kipera katika mfumo mzima wa tashtiti kwa mujibu wa Highet(keshatajwa) ni muhimu kwa kuwasilisha maudhui katika tamthilia *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*.

**Mpomoko**

Baldick (keshatajwa) anaeleza kwamba, mpomoko ni kupotoka ghafla kutoka kwenye hali ya jazba au mhemko hadi hali ya kawaida (isiyo na maana) katika maandishi ya drama, utambaji na maelezo. Athari huwa matokeo yasiyotarajiwa ya kuvunja moyo au taharuki inayoshusha hadhi. Ni hali ambayo inavunja moyo kwa kutokea mwishoni mwa jambo lililokuwa la kuvutia sana au kwa kuwa jambo halijatokea jinsi ilivyotarajiwa. Mfano wa mpomoko katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*:

1) Tamthilia inafika upeo wa juu wakati raia wanafurahi na kumpa hadhi Mkaguzi Mkuu bandia wa Serikali, hali inayovutia mno. Punde tu baada ya hiyo mihemko ya Mkaguzi bandia, ripoti inafika kuwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali aliyetarajiwa kaingia.

   Askari: 'Mtukufu Mkaguzi Mkuu wa Serikali aliyeteuliwa kwa kibali cha Rais amewasili kutoka Pitasbag. Amepanga hotelini na anawahitaji huko mara moja.'

Mpomoko ulioelezwa kwa matukio yanayofuatana na kusadifiana umeonyesha kwa njia iliyo sahili na ya kuchekesha kuwa aliyedhaniwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali (Ghlestakovu) alikuwa tapeli mkuu. Mpomoko huu unazua kicheko kwa kuwa Mkuu wa Wilaya na watu mashuhuri nchini wote wamehadaiwa na mtu mmoja ayari na tapeli ajabu.

Kuwepo matumizi ya tashtiti, mpomoko katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* kunathibitisha kuwa kuna matumizi ya vipengele mbalimbali vya tashtiti katika tamthilia hii. Pia, maudhui yaliyowasilishwa kwa tashtiti hii ni thibitisho la nadharia kuwa tashtiti imetumika kwa namna mbalimbali na mtunzi wa tamthilia kuwasilisha maudhui. Hali hizi mbili zinathibitisha kuwa tashtiti ina umuhimu kama mbinu mwafaka kuwasilisha maudhui.

**Pujufu**

Kamusi ya TUKI (2000) imeeleza kuwa pujufu huhusiana na ng'ono kwa njia ambayo huwachukiza wengi. Maana kamilifu ya akronimu TUKI ni Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili nchini Tanzania, sasa TATAKI yaani Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili. Kuna viashiria au mazungumzo ya simu ambayo ni pujufu. Mfano, kutumia neno matako badala ya makalio au matiti badala ya maziwa. Pujufu pia maana yake ni iliyo kubwa kimaumbile au kisura kiasi cha kupelekea watu wengi kuchukizwa nayo. Mfano, ni pujufu kutumia pesa nyingi sana kwa chakula wakati mamilioni ya watu hawana chakula kabisa. Mifano ya pujufu katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*:

1) Pujufu kuwa Yosif na Ghkestakovu wamekunja mikia kati ya miguu yao kumaanisha wamefilisika sana ni hali ya kitashtiti ambayo inaeleza ukweli wa kifedha kwa wahusika hawa kwa njia ya kuchekesha na isiyoudhi walengwa wa tashtiti.
2) Kauli kuwa Dobchinski anapotoka nyumbani, Hakimu anamwingilia mkewe na eti hakuna mtoto anayefanana na Dobchinski, ila kila mmoja hata yule binti mdogo ni picha kamili ya Hakimu. Inachekesha mno. Tashtiti hii imeeleza kinyaa cha uzinzi pasi kutia chukizo kwa yule anayeambiwa au anayesoma tamthilia.

Kuwepo matumizi ya tashtiti, pujufu katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*, kunathibitisha kuwa kuna matumizi ya vipengele mbalimbali vya tashtiti katika tamthilia hii. Pia, maudhui yaliyowasilishwa kwa pujufu ni thibitisho kuwa tashtiti ina umuhimu kama mbinu mwafaka kuwasilisha maudhui.

**Vurugu**

Hii ni tabia kali ambayo nia yake ni kuua au kuumiza mtu. Pia ni visa vya uvunjaji sheria au vitendo au vitisho vya ukali. Kwa mfano, alishtumu vitendo vya wagomaji kutumia nguvu (vurugu) dhidi ya polisi.

Kipengele cha tashtiti vurugu katika tamthilia *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* kinajitokeza kwa matumizi ya maswali ya balagha na nidaa. Waliomkashifu Mkuu wa Wilaya kwa Ghlestakovu hawakufaulu kwa sababu bintiye Mkuu wa Wilaya, Antoni, alikuwa tayari ameposwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Hali hii inaelezwa kimzahamzaha pasi kuwachukiza walengwa wa tashtiti. Hakuudhi Mkuu wa Wilaya kuwadadisi maadui wake kwa maswali ya balagha na nidaa ifuatavyo:

1) (kwanza kwa upole, halafu kufoka) "…Asante, rafiki zangu. Vipi shughuli? Mu hali gani leo? Salama…? Hamnipendi ehe? Enyi makuli duni! Nyie wavaa magunya! Nyie wanywa gahawa! Enyi wauza marapurapu! Mnathubutu kulalamika juu yangu eh? Enyi viumbe duni, wala makombo, mabeberu! Mlidhania mtaniingiza jela, siyo? Kwa uchawi au kwa mashetani, mimi…!" (Uk. 66)

Mkuu wa Wilaya kwa njia ya vurugu anawacheka waliodhani watamvunjia heshima zake kwa Ghlestakovu. Hawakufua dafu. Matumizi ya kipengele cha tashtiti vurugu katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ni thibitisho kuwa kuna matumizi ya vipengele mbalimbali vya tashtiti katika tamthilia hii kuwasilisha maudhui. Maudhui yaliyowasilishwa kwa kipengele vurugu ni thibitisho kuwa tashtiti ina umuhimu kama mbinu mwafaka kuwasilisha maudhui.

**Uangavu**

Uangavu ni uzuri wa kuelezwa kwa uwazi. Iwapo picha, kitu au sauti ni angavu, unaweza kuiona na kuisikia waziwazi au ukaona waziwazi kupitia kwake. Mifano ya uangavu katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali:*

1) Kwa njia ya uangavu, mtunzi ameonyesha wasiwasi unaomgubika Bwana Posta kabla na baada ya kuifungua barua isiyo yake na tena iliyoandikwa na mtu mashuhuri. Hali hii inazua ucheshi ilhali linaloelezwa ni uozo ulioko katika jamii ambapo anayepewa wadhfa kuchukua barua kutoka posta na kuwakabidhi walengwa zikiwa salama ndiye anayezisoma kisha kuzifunga au kuzituma zikiwa wazi. Tashtiti hii inaeleza ukweli pasi kuudhi anayeambiwa.
2) Pia kuna maelezo kwa uangavu jinsi Mkuu wa Wilaya (Pwagu) alivyopata Pwaguzi-Ghlestakovu. Hali inazua ucheshi ilhali ujumbe uliomo ni majuto makuu ya msemaji baada ya kuhadaiwa na Ghlestakovu, Mkaguzi Mkuu bandia wa Serikali.

Kutokana na tashtiti hii katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*, imethibitika kwamba kuna matumizi ya vipengele mbalimbali vya tashtiti katika tamthilia hii. Pia, kuna maudhui yaliyowasilishwa kwa tashtiti hii, hali inayothibitisha kuwa tashtiti ina umuhimu kama mbinu mwafaka ya kuwasilisha maudhui.

**Chuku**

Baldick (*keshatajwa)* anaeleza chuku kama habari iliyotiwa chumvi. Mfano ni usemi wa kawaida wa kulalamika "nimekuwa nikikusubiri hapa kwa miaka". Kamusi ya karne ya 21 (2011) inaeleza kwamba chuku ni habari iliyotiwa chumvi, maneno ya uongo. Mbatiah (*keshatajwa*) anashadidia kuwa chuku pia huitwa udamisi. Ni tamathali ya usemi inayotumia lugha ya kutilia chumvi aghalabu kwa madhumuni ya kusisitiza. Vile vile chuku ni kauli au maelezo ambayo hufanya kitu kionekane kikubwa zaidi, bora zaidi, baya sana au muhimu zaidi kuliko vile kilivyo. Kwa mfano, ni chuku kusema "ninamjua vyema, nimekutana naye mara mbili". Ufafanuzi huu umedhihirisha kwamba chuku ni kauli iliyoongezewa chumvi. Maana hiii ndiyo iliyozingatiwa katika makala yangu. Mifano ya chuku katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ni kama ifuatavyo:

1) Dondoo lisemalo babake Ghlestakovu angempiga Ghlestakovu kichapo ambacho kingemfanya akune makalio yake kwa Juma zima ni chuku. Pia, ni chuku kusema Yosif ana njaa kiasi cha kumeza dunia. Hali hii kitashtiti inaeleza bila chukizo ubadhirifu wa Ghlestakovu pamoja na tatizo sugu la njaa barani Afrika.
2) Nyama anayopewa Ghlestakovu hotelini ni ngumu kama gome la mti, kavu na haitafuniki. Ugumu huu umetiwa chuku, kuonyesha uduni wa chakula alichopewa. Inachekesha kuwa 'mataya yanauma ukila kipande cha nyama hii….'Hali hii inazua burudani au kicheko.
3) Kusema kuwa Ghlestkovu apewe beseni la maji na mataulo mengi ni chuku. Kauli ya mataulo mengi inachekesha kwa kuwa anayepewa heshima ya kiungu ni mtu duni ambaye aliishiwa na fedha za kujikimu hotelini.

4) Dondoo lisemalo kuwa Ghlestkovu ana nyumba ya kifahari Pitasbag, mpishi, viongozi na mawaziri walio chini yake ni chuku. Ukweli ni kuwa yeye si mtu maarufu kamwe. Hali hii kitashtiti inaeleza ukweli pasi kuchukiza.
5) Dondoo la mwisho ambalo ni kilio cha furaha cha mkewe Luka Lukichi kwa sababu Marya kaozwa Ghlestakovu, linatia ucheshi. Ukweli ni kwamba Ghlestakovu si mtu mashuhuri. Chuku hii imegubika kinaya kilichopo hapa.

Matumizi ya chuku katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ni thibitisho kuwa kuna matumizi ya vipengele vya tashtiti katika tamthilia hii. Mifano ya chuku na maudhui yaliyowasilishwa kwayo inathibitisha kuwa tashtiti imetumika kwa namna mbalimbali na mtunzi kuwasilisha maudhui katika tamthilia *Mkaguzi Mkuu wa Serikali.* Maudhui haya yaliyowasilishwa kwa tashtiti ni ithibati kuwa tashtiti ina umuhimu kama mbinu mwafaka kuwasilisha maudhui.

**Mada za Siku**

Kamusi ya TUKI (2000) imeeleza mada ya siku kama mambo yanayohusiana na wakati unaorejelewa, yaani matukio ya wakati uliopo. Mfano wa mada za siku katika muktadha wa nchi yetu ya Kenya na dunia kwa jumla sasa ni mvuvumko wa janga la Ugonjwa wa Virusi vya Kovidi (UVIKO); chanjo zilizopo kama vile 'AstraZeneca,' 'Pfizer', 'Moderna', 'Johnson na Johnson' pamoja na rai kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kuchanjwa ili kupunguza msambao na makali ya UVIKO endapo watapatwa na janga hili. Mifano ya mada za siku kwa mujibu wa *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ni kama ifuatavyo:

1) Mada za siku-kutowajibika pamoja na wasiwasi ya maafisa wa serikali kukaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ni hali ambayo imeelezwa kisahili na kwa njia ya tashtiti. Haichukizi Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuambiwa "…najua kuwa wewe uko kama sisi wengine na una chembe za udhaifu wako…"
2) Ujanja wa kutapeli umeonyeshwa kimzahamzaha kwa ucheshi. Uzito wa suala hili (utapeli) wakati huo na sasa linasahilishwa kupitia hii mizaha. Ghlestakovu anafurahi kupata shilingi 400 kutoka kwa Hakimu, 400 kutoka kwa Bwana Afya na 400 kutoka kwa Mratibu wa Elimu. Hali hii inachekesha ilhali ujumbe ulioshehenwa ni nyeti yaani utapeli.

Kipengele cha tashtiti, mada za siku, kimetumiwa katika tamthilia *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* kuwasilisha maudhui nyeti ya kuchukiza pasi kuchukiza msomaji au mtazamaji wa tamthilia. Hali hii inadhihirisha kuwa tashtiti ina umuhimu kama mbinu mwafaka ya kuwasilisha maudhui.

**Hitimisho**

Tashtiti kupitia vipengele 10 imetumika kwa ufundi mkubwa kuelezea maudhui nyeti katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* kama vile, ufisadi, kutowajibika kwa viongozi katika nyadhfa zao mbalimbali, ubadhirifu wa mali ya umma, uozo katika jamii (barua kufunguliwa na Bw. Posta) kufuja mali, uzinzi, unafiki, utapeli, madhara ya ulevi, tatizo sugu la njaa Afrika, ujinga (Ghlestakovu kudhaniwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kupewa heshima ya kiungu) na malezi duni (Ghlestakovu kudekezwa na babake mzazi). Utumiaji wa tashtiti katika kuelezea maudhui umeweka wazi mambo mazito kwa mguso hafifu wa kihisia ambao hauchukizi msomaji. Maudhui haya yameelezwa kikamilifu na kimzaha kupitia tashtiti na vipengele kumi vilivyotaja.

**Marejeleo**


Ayodi, N.K. (2011). Matumizi ya Tashtiti katika Tamthilia Teule za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Ayodi, N.K. (1997). Mbinu za Kistanislaviski katika Tamthilia ya Tahamaki; 'Likizo', Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

Baldick, C. (2001). *Oxford Dictionary of Literary Terms*. New York: Oxford University Press.

Gogol, N. (1979). *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*. Nairobi: East African Education Publishers.

Highet, G. (1962). *The Anatomy of Satire*. Princeton: Princeton University Press.

Imbuga, F. (1994). *Usaliti Mjini*. Nairobi: East African Education Publishers Limited

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Longsworth, R. (1973). *The Design of Drama*. West Haven: Pendulum Press Inc.

Mbatiah, M. (2000). *Kamusi ya Fasihi*.Nairobi: Standard Text Books Graphics & Publishing.

Murungi, J.M., Matundura, E., na Rori, Z.N., (2011) Wahariri wakuu *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja*. Nairobi: Longhorn Publishers.

TUKI (2000). *English -Swahili Dictionary 2nd Edition*. *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili Toleo la Pili*. Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam. Mauritius: Book Printing Services Ltd.